Australian Government
AUSTRAC

FIGHTING FINANCIAL CRIME TOGETHER


# Mbinu za kupunguza hatari

## Taarifa muhimu kwa watoa huduma za kifedha

***Sheria ya Kupambana na Utakatishaji Fedha na Kukabiliana na Ugaidi* 2006 (AML / CTF Act) hutoa uhuru kwa wafanyabiashara kudhibiti hatari zao. Inaweka imani kubwa kwa wafanyabiashara kutambua na kudhibiti hatari zao, kwa hivyo wafanyabiashara lazima waonyeshe kuwa wanachukua jukumu hili kwa uzito.**

### Muhtasari wa mbinu

Mbinu za usimamizi wa hatari zina vipengele vinnemuhimu. Ni mchakato unaoendelea:




1. Tambua hatari. Zingatia wateja wako, bidhaa na huduma unazotoa, jinsi unavyotoa bidhaa zako, na wapi unafanya biashara.

2. Kwa kila hatari iliyotambuliwa, fikiria uwezekano wa kutokea na kiwango cha athari inaweza kuwa nayo. Tathmini na toa kipaumbele kwa kila hatari kulingana na mambo haya. Fikiria athari kwa biashara yako, sekta nzima na Jamii nzima ya Australia.

3. Tekeleza vidhibiti vya kusimamia hatari ulizozitambua. Hakikisha unabainisha vitendo hivi na vidhibiti katika mpango wako wa AML / CTF. Kumbuka kwamba udhibiti wako utakuwa na ufanisi ikiwa una tathmini thabiti za hatari.

4. Endelea kufuatilia ufanisi wa vidhibiti vyako katika kusimamia hatari. Hakikisha mara kwa mara unakagua hatari na vidhibiti vyako ili kuendana na mabadiliko.

## MIFANO YA VIGEZO VYA KUZINGATIA

Unatuma pesa kwenda nchi zipi?

Je! Unahamisha pesa kwa wengine, unakubali pesa kutoka kwa wengine, au vyote viwili?

Unakubali aina gani za njia za malipo?

Je! Miamala inafanyika inafanyika ana kwa ana ama mtandaoni?

Je! Una vikomo vya miamala?

Je! Miamala ya wateja wako ni ya mtindo gani?

Una wafanyikazi, au unakamilisha miamala yote wewe mwenyewe?

Wateja wako, wako wapi?

## HATARI ZINAZOWEZA KABILI BIASHARA YAKO




## KUTATHMINI HATARI

Wakati wa kutathmini utakatishaji fedha, ufadhili wa ugaidi na hatari zingine za uhalifu kwenye biashara yako lazima uzingatie hatari zinazosababishwa na sababu nne zifuatazo:

- Wateja wako
- Bidhaa na huduma
- Njia za utoaji huduma
- Mamlaka

## Ukadiriaji wa hatari

Wakati wa kutathmini na kuweka vipaumbele katika hatari, tathmini yako ya hatari hizi lazima iamue kiwango cha hatari kwa kila aina ya huduma unayotoa (kwa mfano: juu, kati, chini).

Sehemu muhimu ya mpango wako wa kufuata AML / CTF, ni kupunguza hatari inayosababishwa na wateja au miamala yenye hatari kubwa..

## Kudhibiti hatari ni muhimu kulinda biashara yako

Tathmini thabiti ya hatari, mpango wa ufuatiliaji wa miamala na mpango wa kufuata AML / CTF ni muhimu kulinda biashara yako kutumika kijinai.

**Udhibiti wa hatari ni mchakato endelevu. Mara kwa mara ni lazima upitie na usasishe tathmini yako ya hatari.**

Mchakato wako wa kutathmini ya hatari lazima uandikwe na kusahihishwa kama inavohitajika.Unahitaji kufanya tathmini ya hatari kabla ya kutoa bidhaa au huduma mpya, au wakati wowote yanapotokea mabadiliko kwenye bidhaa iliyopo ambayo hubadilisha hatari yake.

Kwa mifano ya hatari kadhaa unazoweza kukumbana nazo na vitendo unavyoweza kuzingatia, angalia **karatasi ya viashiria vya hatari kwa watoa huduma za kutuma pesa.**

Mwongozo wetu maalum wa sekta ya watoa huduma za utumaji fedha pia hutoa habari juu ya jinsi ya kutengeneza mpango wa AML / CTF.

Kwa taarifa zaidi, ingia **austrac.gov.au/remittance-service-providers**

D1014